pdfeducation.com

Jina: _____ Namba ya Mtahiniwa: _____

1410/206
KISWAHILI
Juni/ Julai 2015
Muda: Saa 3

Sahihi ya Mtahiniwa: _____

Tarehe: _____

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

NATIONAL CERTIFICATE IN SOCIAL DEVELOPMENT

KISWAHILI

Saa 3

MAAGIZO

Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
*Mtihani huu una sehemu **NNE** muhimu. **INSHA, UFAHAMU, MATUMIZI YA LUGHA NA MBINU** na **VIFAA VYA KUFUNDISHIA.***
*Jibu maswali **yote**.*
Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.
Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

Kwa Mtahini Pekee

Sehemu	Swali	Upeo	Alama
A	1	20	
B	2	30	
C	3	30	
D	4	20	
	JUMLA	100	

Karatasi hii ina kurasa 16 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

© 2015 The Kenya National Examinations Council

Fungua ukurasa

pdfeducation.com

SEHEMU A: INSHA (alama 20)

1. *Andika insha isiyopungua kurasa mbili wala kuzidi kurasa mbili na nusu juu ya mojawapo wa vichwa vifuatavyo:*

   (a) Ushikwapo shikamana.

   (b) Kamati inayoshughulikia macndeleo ya vijana katika wilaya yako imekuwa na mkutano hivi karibuni. Ukiwa katibu wa kamati hiyo, andika kumbukumbu za mkutano huo.

   (c) Wewe ni mwenyekiti wa chama cha wafanyakazi katika kampuni yenu. Andika barua kwa mkurugenzi wa kampuni kuyaeleza matatizo yenu.

   (d) "Kuwepo kwa televisheni katika maisha yetu kumevuruga mshikamano wa jamaa katika jamii kwa kiasi kukubwa." Jadili.

   (e) Toa ushauri wako kwa serikali kuhusu jinsi inavyoweza kukabiliana na tatizo la ulanguzi wa dawa za kulevya.

SEHEMU B: UFAHAMU (alama 30)

2. *Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo.*

Ochieng alienda kama mwanajeshi wa kisasa. Kwiliwili chake kirefu hakikubyonga wala kudhoofu hata kidogo, kilikuwa mwimo wa ushupavu mwingi. Kwa takribani miaka kumi, alikuwa amekwaruzana na mazingira makali ya kazi na maisha. Kila uchao aliitwa ili kusuluhisha ugomvi baina ya wazazi wasiosikilizana kwa ulevi na uhaba wa pesa. Nyakati nyingine aliitwa ili atoe nasaha kwa vijana waliotunduka. Vijana kama hawa walimkera na kumghasi kwa sababu ya utovu wa heshima na adabu. Hata hivyo, alijitolea kuwakanya na kuwaonyesha njia yenye natija maishani mwao. Usiku angeamshwa na fujo na ghasia za majirani wasiojua kusuluhisha matatizo yao kwa upole. Ochieng aliishi katika mazingira yasiyojua utulivu wala simile.

Mfanyakazi huyu aliheshimiwa na wengi lakini kama ilivyo kawaida ya mahuluki, hapakukosa wachache waliomuonea kijicho cha sifa zake nzuri za uongozi na hisia za kibinadamu zisizo kifani. Kuna wale waliomchukia kwa sababu hakuvuta sigara wala kuzubaa mitaani. Pia kuna wale waliotuhumu kwamba alikuwa na madhumuni fulani ya kibinafsi aliyoyaficha. "Kwa nini iwe yeye kila siku?" Waliuliza.

Wengine walimdharau kwa bidii zake. Viongozi fulani mtaani walikerwa na kukereketwa kwa sababu alikuwa mtetea mazingira aisyemithilika wala kutetereka. Ochieng alimwambia kila aliyejali kusikia kwamba mazingira mazuri ndiyo msingi wa maisha mema.

Asubuhi hiyo hatua zake zilikuwa ndefu na imara. Alikwenda chapuchapu huku akitua ardhini kwa kishindo kama kwamba alitaka kujua udhabiti wake. Alikuwa na ujasiri mwingi na dhamira isiyotikisika.

pdfeducation.com

Lengo la Ochieng siku hiyo lilikuwa kumweleza mwajiri wake yote yaliomkaa moyoni. Alikusudia kumpasulia mbarika kumwambia kwamba endapo kampuni yake haitafanya juhudi kulinda mazingira na kupunguza uchafuzi wake utokanao na viwanda vyao, basi wafanyakazi hawatakuwa na jingine la kufanya ila kuitisha mgomo.

Wafanyakazi wote waliafikiana kuwa maisha ya watoto wa Kaloleni yalikuwa hatarini kutokana na shughuli za "Exploit and Dump International " (EDI). Viwanda vya EDI vilitoa wingu jeusi la moshi usiku na mchana. Isitoshe, viliteuka harufu mbaya mithili ya mzoga uliooza ukaozeana na kuvundiana. Hewa hiyo chafu ilivutwa na wakazi wa Kaloleni. Watoto waliteuka, waliteuka harufu mbaya ya viwanda vya EDI.

Wakurugenzi wa viwanda vya EDI hawakujali asilani kuhusu maslahi ya wananchi. Walikata misitu bila kusaza wala kupanda miti mingine. Ute uliwadondoka na kuwachurazika chururu walipoona malighafi tele iliyokuwa imewazingira. Wakaiparamia kwa ubinafsi mwingi.

Takataka kutoka viwandani ilitupwa ovyo ovyo karibu na nyumba za watu; maji machafu yalielekezwa barabarani yachezewe na watoto; na mashine viwandani zilitoa kelele kalikali mchana kutwa na usiku kucha hivi kwamba wakazi wa Kaloleni walikuwa hatarini ya kuwa viziwi. Hata hivyo, wakurugenzi hawakujali kwa sababu miradi yao litekelezwa kulingana na maagizo yao. Walikuwa na alaka nzuri na asasi za kitawala zilizowahami pindi walipojikuta matatani. Daima walitumia fursa yoyote waliyopata kudhulumu na kubainisha ufidhuli wao kwa wenyeji wa Kaloleni.

Mtoto wa Ochieng alikuwa ameshikwa na ugonjwa wa kukohoa na kuchubuka ngozi. Daktari alisema kuwa ugonjwa huo ulitokana na sumu kali ya viwanda. Usiku kucha Ochieng alisikiliza kikohozi hicho cha msinga kilichomkejeli. Maradhi ya mwanawe yalimtilifu sana.

Ochieng alikaza mwendo. Japo alikuwa mtetea mazingira na haki za wafanyakazi kwa muda mrefu, sasa alikuwa na sababu kubwa zaidi ya kuwakabili viongozi wa EDI. Imani yake ilikuwa kubwa na thabiti zaidi.

(a) Ipe habari uliyoisoma kichwa kifaacho. (alama 2)

(b) Taja hulka mbili zilizomsaidia Ochieng kuyakabili mazingira yake. (alama 2)

(c) Mhusika Ochieng alikwaruzana na makali gani katika kazi na katika maisha? (alama 3)

(d) Watu wengi walimstahi Ochieng. Eleza ni kwa nini. (alama 4)

(e) Ni dhamira gani iliyomfanya Ochieng kwenda kwa mwajiri wake? (alama 3)

(f) Eleza ni vipi maisha ya watoto wa Kaloleni yalikuwa katika hatari. (alama 3)

(g) Toa sababu zako kuwa "Wakurugenzi wa EDI hawakujali maslahi ya wananchi." (alama 5)

(h) Mwandishi anamaanisha nini anaposema:

(i) Atoe nasaha kwa vijana waliotunduka. (alama 2)

pdfeducation.com

(ii) Asiyemithilika wala kutetereka. (alama 2)

(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa: (alama 4)

(i) kumpasulia mbarika;

(ii) watoto waliteuka;

(iii) zilizowahami;

(iv) yalimtilifu.

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA (alama 30)

3. Jibu maswali yote.

(a) Zirekebishe sentensi zifuatazo:

(i) Tafathali ripa kabra ya kura. (alama 1)

(ii) Mbuzi ya papa yangu imekufa. (alama 1)

(b) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi:

(i) Waraka ambao umeandikwa ni wa Fatuma. (alama 2)

(ii) Uzee ambao unasikitisha ni ule wa upweke. (alama 2)

(c) Panga nomino zifuatazo katika ngeli zake tofauti.

(i) rafiki
(ii) mwezi
(iii) kuabudu
(iv) Indonesia.

(alama 4)

(d) Tumia kinyume cha kitenzi ulichopewa katika sentensi.

(i) ficha. (alama 2)

(ii) kama (alama 2)

(e) Tunga sentensi zenye mpangilio ufuatao wa maneno:

(i) Nomino kivumishi kitenzi kielezi kielezi. (alama 2)

pdfeducation.com

(ii)

S			
KN	KT		
N	T	N	E

(alama 2)

(f) Onyesha viambishi awali na tamati katika maneno haya:

(i) watatukaribisha; (alama 2)

(ii) wamewasamehea. (alama 2)

(g) Tofautisha sentensi hizi kimaana:

(i) Gari liliibwa. (alama 1)

(ii) Gari liliibiwa. (alama 1)

(h) Akifisha sentensi zifuatazo:

(i) je utaenda kwao siku ya alhamisi. (alama 1)

(ii) ala mkono mtupu haulambwi askari akasema. (alama 2)

(i) Watu wafuatao waitwaje?

(i) Mwanamke mwenye miba. (alama 1)

(ii) Mwanamume mzee sana. (alama 1)

(j) Taja methali inayoweza kukamilisha maelezo haya: (alama 1)

Aambiwaye methali hii ni mtu anayestaajabu ni kwa nini fulani aliyezoea uzungu, kwa mfano, amerudi kijijini mwao.

pdfeducation.com

SEHEMU D: MBINU NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA

Jibu Maswali yote

4. (a) Wewe kama afisa anayeshughulikia maslahi ya jamii katika kata yako, umetembelea vikundi vya akina mama na umepata kuwa wanakabiliwa na changamoto mbalimbali. Andika ripoti utakayowasilisha kwa afisa mkuu wa jamii katika wilaya yako.

(alama 10)

(b) Ukiwa kiongozi wa kikundi cha vijana cha "Jitegemee", andika mchezo wa kuigiza utakaogizwa na kikundi chako katika tamasha za kuleta amani na utangamano miongoni mwa vijana kutoka makabila tofauti wanaoishi kijijini mwako.

(alama 10)